TANGAZO LA SERIKALI NA. 271 la tarehe 12/4/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA AFYA, USAFI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya wilaya ya Songwe ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Songwe.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma ya kuzoa taka;

"adha" maana yake ni hali yoyote mbaya yenye kuleta madhara juu ya afya ya watu na viumbe hai kwa ujumla;

"afya" maana yake ni hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii na wala si tu kutokuwa na ugonjwa au kilema;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa na

binadamu na inajumuisha maji na dawa;

"chanzo cha maji" maana yake ni eneo lolote ambalo limetengwa kwa ajili ya kuwa chanzo cha maji kwa matumizi ya jamii ikiwemo visima, mito, chemchemi, vijito, na maeneo yote yanayopatikana maji;

"choo bora" maana yake ni choo chochote cha maji chenye sakafu inayosafishika, banda imara la kudumu, limeezekwa, lina mlango imara, bomba la kutoa hewa chafu na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwa kwa vifaa vya kudumu;

"chukizo la kiafya" maana yake ni kitu chochote kinachoweza kuleta kinyaa machoni kwa kuona, kunusa, hewa chafu, madhara au kuhatarisha afya za binadamu na wanyama;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Songwe;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi; mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa chini ya Sheria Ndogo hii au Sheria nyingine yoyote;

"jengo la biashara" maana yake ni jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya biashara iliyokusudiwa;

"kaya" maana yake mtu mzima anayejitegemea mwanamke au mwanaume, na mtoto au watoto inayoishi aidha kwenye nyumba nzima au ndani ya chumba kimoja kwenye eneo la Halmashauri;

"kelele" maana yake ni kero inayosababishwa na sauti ambayo kwa asili inakataliwa au inaweza kusababisha athari mbaya kwa afya ya binadamu au

mazingira;

"kero" au "chukizo" maana yake ni kitu chochote kilicho katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni kichafu kiasi cha kusababisha-

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu;

(b) harufu mbaya au harufu ya kuudhi au kuleta kinyaa;

(c) kuzaliana kwa wadudu hatari kama vile inzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"kikundi cha mazingira" au "kikundi cha usafishaji" maana yake ni kikundi chochote cha watu kilichosajiliwa kufanya usafi na usimamizi wa mazingira na udhibiti wa uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Halmashauri;

"mabwawa ya maji taka" maana yake ni mabwawa yaliyojengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi na kutakasa maji taka yanayotokana na kuosha vyombo, kutoka vyooni, kutoka bafuni, kufua nguo, kuosha nywele au shughuli zozote za nyumbani na viwanda;

"magonjwa ya mlipuko" maana yake ni magonjwa yanayotokea kwa muda mfupi ya kuambukiza na kuenea kwa haraka na kuathiri watu wengi ndani ya muda mfupi yanayoweza kutolewa amri ya taadhari;

"maji taka" maana yake ni maji yenye mchanganyiko wa kinyesi, mkojo, na maji kutoka masinki ya kuogea,

kutema mate na kunawia mikono, pamoja na maji yenye mchanganyiko wa vitu vingine vyenye asili ya chemikali au visivyo na chemikali;

"mazalia ya wadudu" maana yake ni sehemu ambayo wadudu hufanya mazalio au kuishi kwa minajiri ya kufanya mzunguko wa maisha na baadae kuleta maadhara kwa binadamu;

Sura ya 323

"mazao ya misitu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu;

"mazingira" maana yake ni masuala yote yanayohusisha maumbile halisi yanayowazunguka binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia ya nchi, sauti, mwanga, harufu, radha, vijiumbe, hali za kibaiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na binadamu na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana;

"mifugo" maana yake ni ng'ombe, punda, nguruwe, mbuzi, mbwa, kondoo, kuku na wanyama wengine wote wanaofugwa majumbani;

"mgahawa" maana yake ni shughuli zote za uuzaji wa chakula na vinywaji zinazofanyika katika sehemu ya nje ya jengo maalumu la mgahawa au hoteli;

"misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 na miti, uoto wa asili au uliopandwa, au asilimia 50 au zaidi ya vichaka na miti inayoota au ambayo itajumuisha na yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangaza chini ya sheria za misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe au Afisa yeyote aliyeteuliwa

kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hii;

"mzalishaji wa maji taka" maana yake ni mtu, shirika, kiwanda au taasisi ambapo shughuli zake kwa namna yoyote zinazalisha maji taka;

"taka" maana yake ni kitu chochote ambacho baada ya kukitumia hakina thamani kwa wakati huo na uwepo wake katika eneo hilo unaweza kusababisha chukizo la kiafya na kuhatarisha afya ya jamii;

Sura ya 191

"taka hatarishi" maana yake ni kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"taka za biashara" maana yake ni aina yoyote ya taka ambazo hupatikana au hutokana na shughuli mbalimbali za kibiashara;

"taka ngumu" maana yake ni kitu chochote ambacho baada ya kukitumia hakina thamani yoyote kwa jamii inayohusika, uwepo wake katika eneo husika unaweza kusababisha machukizo ya kiafya na kuhatarisha afya ya jamii;

"taka za majumbani" maana yake ni mabaki ya vyakula, maganda ya matunda, majivu, nguo chakavu, karatasi za aina mbalimbali, kinyesi cha mifugo, taka za bustani na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;

"taka za viwandani" maana yake ni aina yoyote ya taka ambazo hutokana na uzalishaji wa shughuli mbalimbali viwandani;

"ugonjwa wa kuambukizwa" maana yake ni ugonjwa wowote unaoweza kuambukizwa kutoka kwa mtu na mtu, mtu kwa mnyama au mtu kwa mdudu;

"vitu hatari" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa

niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Mamlaka ya Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kufanya yafuatayo:

(a) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za usafi afya na mazingira;
(b) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kufuata kanuni za afya, usafi na kutunza mazingira;
(c) Kuteua mtu yeyote, wakala, kikundi au taasisi kutekeleza shughuli za usimamizi wa afya, usafi na mazingira kwa niaba ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) Kufanya ukaguzi ili kubaini endapo kanuni za afya, usafi na utunzaji wa mazingira zinazingatiwa ndani ya eneo la Halmashauri;
(e) Kumchukulia hatua za kisheria mtu yoyote anayekiuka Sheria Ndogo hii au Sheria nyingine inayohusiana na afya, usafi na usimamizi wa mazingira zilizotungwa na Bunge;
(f) Kutunga kanuni, miongozo au kutoa maelekezo yatakayosaidia kulinda afya, usafi na usimamizi wa mazingira ndani ya eneo la Halmashauri; na
(g) Kuingia mkataba na mtu yeyote, taasisi au kampuni kutelekeza shughuli za usimamizi wa afya, usafi na mazingira kwa niaba ya Halmshauri katika eneo ndani ya Halmashauri.

Usafi wa mazingira

5.-(1) Kila mkazi au mfanyabiashara anayemiliki jengo au eneo la biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba:

(a) majani yanayozunguka jengo lake au makazi yanakatwa au kupaliliwa na kuondolewa katika eneo lake lote;
(b) taka ngumu zote ikiwa ni pamoja na mifuko ya

plastiki zinakusanywa, kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;

(c) maji taka yanaelekezwa ndani ya mfumo wa maji taka;

(d) anaboresha na kupaka rangi jengo lake kila inapochakaa;

(e) anakuwa na choo kilicho bora na kisafi wakati wote;

(f) anashiriki siku ya usafi ya Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi;

(g) anaondoa uchafu ikiwemo mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo katika mfereji wa maji ya mvua inayomzunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mifereji hiyo inakuwa safi wakati wote;

(h) hakuna mkusanyiko wa maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuathiri upitishaji wa maji ya mvua na hivyo kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla;

(i) anafanya uchambuzi wa taka;

(j) ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili kuhifadhi taka ngumu kabla hazijachukuliwa kwa ajili ya kwenda kutupwa katika eneo lililotengwa kwa ajili ya kuhifadhi taka;

(k) anatunza na kuhifadhi vyombo vya kuhifadhia taka vinavyowekwa na Halmashauri;

(l) kwa mfanyabiashara wa matunda au miwa, ana chombo maalumu cha kuhifadhi maganda au mabaki ya matunda.

Ada ya uzoaji taka

6.-(1) Kutakuwa na ada ya uzoaji taka ambayo itatozwa na Halmashauri kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa mazingira kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Ada ya uzoaji taka italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika na italipwa kwa Afisa Mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo kwa njia ya kieletroniki na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka.

(3) Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Udhibiti wa kelele kwa shughuli mbalimbali za kijamii

7. Mtu yeyote haruhusiwi kusababisha au kufungulia kelele kupita kiasi iwe muziki, kelele za kiwanda, jenereta au kitu kingine chochotebila kupata kibali cha Afisa Mwidhiniwa.

Kutiririsha maji taka

8.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa, wakati wa mvua au wakati wowote, kutiririsha, kumwaga, kuruhusu au kusababisha kutiririsha au kumwaga maji taka au kinyesi kutoka chooni au sehemu yoyote barabarani, uchochoroni, kwenye mifereji ya maji ya mvua, kwenye vyanzo vya maji au sehemu yoyote isiyotengwa kwa ajili ya kuhifadhi maji taka.

(2) Kila kiwanda kinachozalisha maji taka kitakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa kinaunganisha maji taka au kujenga mifereji na mabwabwa kwa ajili ya kuhifadhi maji taka.

(3) Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo la kuhifadhi linapojaa

Taka za viwanda

9.-(1) Ni wajibu wa kila mwenye kiwanda kuhakikisha kuwa taka kama vumbi, maganda, moshi na taka nyingine zinazoweza kuleta kero au adha kwa ujumla haziwafikii au kuleta madhara kwa binadamu na viumbe hai wengine.

(2) Ni marufuku kwa kiwanda chochote kutoa au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu au harufu mbaya, vumbi au kelele na kusababisha kero kwa wakazi.

Taka hatarishi

10. Ni marufuku kwa mtu yeyote, kampuni, wakala au taasisi kuendesha shughuli za uchomaji wa taka hatarishi bila kupata kibali kutoka Halmashauri.

Utengenezaji na uuzaji wa vyakula

11. Mtu yeyote hataruhusiwa kutengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za afya.

Uuzaji wa vyakula vilivyopikwa

12.-(1) Kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao safi na kuwekwa kioo kinachozuia inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote-

(a) kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini, vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza;

(b) kupanga vyakula nje ya duka la vyakula; na

(c) mfanyabiashara, hospitali, taasisi, kaya, jengo au shughuli za viwanda kuchafua anga hewa kwa kuachilia moshi angani unaoweza kuleta madhara kwa binadamu, mimea na viumbe hai.

Usalama wa matumizi ya maji

13.-(1) Kila mkazi anapaswa kuhakikisha kwamba maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama bila kujali chanzo chake.

(2) Kila mmiliki wa kisima atapaswa kuhakikisha maji ya kisima yanapimwa ili kuwa salama kwa matumizi.

Uzuiaji wa shughuli wakati wa magonjwa ya mlipuko

14. Mkurugenzi anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.

Ukamataji wakati wa zuio

15.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kumkamata mtu yeyote ambaye atakaidi amri ya zuio la kufanyika kwa shughuli ya uuzaji wa vyakula wakati wa magonjwa ya mlipuko.

(2) Endapo mtu aliyekamatwa alikuwa anauza vyakula ambavyo vinaharibika kwa haraka Halmashauri itaharibu vyakula hivyo.

(3) Bila kuathiri aya ndogo za (1) na (2), endapo vyakula vilivyokamatwa vitakuwa haviharibiki kwa haraka Halmashauri itakuwa na jukumu la kuvihifadhi hadi mwisho wa amri ya zuio.

(4) Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa kwa uzembe wa Afisa wa Halmashauri.

Upimaji wa afya

16.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mhudumu wa hoteli, migahawa, baa, bucha, sehemu za kuoka mikate, nyumba za kulala wageni, grosari au mtu yeyote

anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza kupima afya kila baada ya miezi sita.

(2) Itakuwa ni kosa kwa mmiliki yeyote kuruhusu mhudumu yeyote kufanya kazi bila kupima afya yake.

Uwezo wa kukagua

17.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote muda wowote kukagua utekelezaji wa Sheria hii wakati wa saa za kazi na wakati wowote inapotakiwa kufanyika kwa ukaguzi maalumu.

(2) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.

Udhibiti wa ubebaji kokoto, mawe na mchanga

18. Mtu yeyote atakayesafirisha mawe, mchanga au kokoto katika eneo la Halmashauri atahakikisha kuwa chombo anachotumia kusafirisha kimefunikwa ili kuzuia kumwagika na kuchafua mazingira.

Mabaki ya ujenzi

19. Mtu yeyote hataruhusiwa kubomoa au kusababisha kubomoka kwa jengo au sehemu ya jengo bila kutoa taarifa kwa Halmashauri na kulipa gharama kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

Udhibiti utupaji wa taka

20.-(1) Watumiaji wa vyombo vya usafiri binafsi au vya umma hawataruhusiwa kutupa taka nje ya vyombo wanavyotumia na taka zote zitawekwa kwenye chombo cha kuhifadhia taka kilichomo kwenye chombo cha usafiri husika.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa taka ovyo katika maeneo ya makazi, biashara, mifereji ya maji ya mvua, hifadhi ya barabara au mahali popote pasipotengwa kwa ajili ya kutupa taka.

(3) Mtu yeyote atakuwa na wajibu wa kuhakikisha

kwamba anatupa uchafu au taka katika vyombo maalumu vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalumu yaliyotengwa.

Uanzishwaji wa Vikundi Jamii

21. Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa Vikundi Jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

22. Kila mmiliki wa nyumba au mpangaji atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba-

(a) nyumba yake ina choo safi, imara kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo;
(b) anaweka sehemu maalumu ya kunawia mikono ikiwa na maji safi na sabuni ya kimiminika; na
(c) choo kinajengwa umbali wa mita sitini kutoka chanzo chochote cha maji.

Vyoo vya umma

23.-(1) Halmashauri inaweza kujenga choo cha umma au kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya umma katika maeneo ambayo Halmashauri itaona inafaa.

(2) Vyoo vitakavyojengwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii vitakuwa vya kudumu na:

(a) matundu yasiyopungua mawili kwa wanawake na mawili kwa wanaume;
(b) mfumo madhubuti wa maji na uwepo wa maji ya kutosha yaliyo safi na salama;
(c) kuwa na chombo cha kuhifadhi maji ya akiba;
(d) kuwa na bafu ya wanaume na wanawake;
(e) kuwa na chumba maalumu cha kuvutia sigara;
(f) kuwa na sehemu ya haja ndogo kwa wanaume;

(g) kuwa na chombo maalumu chenye mfuniko cha kuhifadhia taka zisizoweza kusukumwa na maji.

Vyoo vya muda katika mikusanyiko

24. Ni wajibu wa mtu yeyote, kikundi au taasisi yenye lengo la kukusanya watu kwa madhumuni ya mkutano, sherehe au mkusanyiko wowote kuweka au kujenga vyoo vya muda baada ya kuomba idhini kutoka Halmashauri endapo katika eneo husika hakuna choo cha kudumu.

Vyoo katika majengo ya biashara

25. Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hii kwa ajili ya matumizi ya wateja wake kwa kuzingatia jinsi zote.

Ilani ya kujenga au kurekebisha choo

26. Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo.

Ilani ya kuondoa kero

27.-(1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ndani ya siku saba kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.

Uteuzi wa Wakala

28.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Wakala wa kukusanya ada kwa niaba yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala atakayeteuliwa chini ya Sheria hii atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya, kwa niaba ya Halmashauri, ada mbalimbali zinazohusiana na afya, usafi na usimamizi wa mazingira, katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hii;
(b) kukusanya ada kwa kutumia mfumo wa kielekitroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri; na
(c) kutekeleza masharti yote ya mkataba.

Makosa

29. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-
(a) atatupa taka au uchafu wowote au kuacha takataka au uchafu kwenye nyumba, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara au eneo linalopakana na nyumba yoyote au ardhi yoyote au karibu na maeneo ya nyumba au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo;
(b) atamzuia au kujaribu kumzuia au atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii;
(c) atamwaga taka barabarani, katika mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni au mahali popote hadharani au katika eneo lolote lisiloruhusiwa;
(d) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;
(e) atatiririsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;
(f) ataosha magari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;
(g) atapika vyakula pembezoni mwa barabara au nje

ya majengo mengine;

(h) atauza vyakula maeneo yasiyo rasmi na kushindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;

(i) atafanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo, katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(j) atavuta sigara hadharani au mahali pa jumuiya au kwenye vyombo vya usafiri;

(k) atatema mate ovyo au kutema mate barabarani au mahali pa jumuiya;

(l) ataacha nyumba anayoishi, anayomiliki au kufanyia shughuli zake katika hali ya uchafu yenye kuleta kero au chukizo;

(m) ataacha chombo cha usafiri katika hali ya uchafu;

(n) ataendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(o) ataanzisha au kufungua karakana katika majengo au majumba au maeneo ya makazi;

(p) ataenda haja ndogo au kubwa ovyo barabarani, uchochoroni au upenuni; au

(q) atafanya biashara ya kuosha gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo au kuruhusu eneo lake kutumika kwa shughuli za kuosha vyombo vya moto katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hizo bila kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.

Adhabu

30. Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

31. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 6(1))*

SEHEMU A:

ADA YA UZOAJI WA TAKA

| Namba. | Aina ya Biashara | Viwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Makazi (Kaya) | 3,000/= kwa mwezi |
| 2 | Mgahawa Mdogo | 5,000/= kwa mwezi |
| 3 | Mgahawa Mkubwa | 15,000/= kwa mwezi |
| 4 | Nyumba ya kulala wageni | 10,000/= kwa mwezi |
| 5 | Zahanati (Taka zisizo hatari) | 5,000/= kwa mwezi |
| 6 | Hospitali | 10,000/= kwa safari |
| 7 | Kiwanda cha Kuuza Mbao | 10,000/= kwa mwezi |
| 8 | Fundi Selemala Wakubwa | 30,000/= kwa mwezi |
| 9 | Fundi Selemala wa Kati | 20,000/= kwa mwezi |
| 10 | Fundi Selemala Wadogo | 5,000/= kwa mwezi |
| 11 | Fundi Chuma | 15,000/= kwa |

| | | |
|---|---|---|
| | | mwezi |
| 12 | Karakana | 20,000/= kwa mwezi |
| 13 | Kiwanda kidogo | 50, 000/= kwa mwezi |
| 14 | Kiwanda Kikubwa | 200,000/= kwa mwezi |
| 15 | Duka la Jumla | 10,000/= kwa mwezi |
| 16 | Duka la rejereja/huduma | 5,000/= kwa mwezi |
| 17 | Shule ya msingi ya Bweni (Binafsi) | 20,000/= kwa mwezi |
| 18 | Shule ya Msingi ya Kutwa (Binafsi) | 10,000/= kwa mwezi |
| 19 | Shule ya Sekondari ya Bweni(Binafsi) | 30,000/= |
| 20 | Shule ya Sekondari ya kutwa(Binafsi) | 15,000/= kwa mwezi |
| 21 | Kituo cha kulea watoto | 5,000/= kwa mwezi |
| 22 | Kituo cha kutunzia watu wenye mahitaji maalumu | 5,000/= kwa mwezi |
| 23 | Duka dogo la Chakula | 5,000/= kw3a mwezi |
| 24 | Duka kubwa la chakula | 10,000/= kwa mwezi |
| 25 | Baa | 10,000/= kwa mwezi |
| 26 | Klabu ya Usiku | 10,000/= kwa mwezi |
| 27 | Kumbi za Sherehe | 20,000/= kwa mwezi |
| 28 | Duka la kuuza Nyama na Samaki | 10,000/= kwa mwezi |
| 29 | Dukala Dawa (jumla) | 10,000/= nkwa mwezi |
| 30 | Dobi Mdogo | 3,000/= kwa mwezi |
| 31 | Dobi Mkubwa | 5,000/= kwa mwezi |
| 32 | Fundi wa vifaa vya Umeme | 5,000/= kwa mwezi |
| 33 | Fundi Cherehani | 5,000/= kwa mwezi |
| 34 | Saluni | 5,000/= kwa mwezi |
| 35 | Kituo cha kuuza mafuta | 10,000/= kwa mwezi |
| 36 | Stoo | 5,000/= kwa mwezi |
| 37 | Ghala | 10,000/= kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| 38 | Hoteli | 20,000/= kwa mwezi |
| 39 | Taasisi | 20,000/= kwa mwezi |
| 40 | Klabu ya pombe za asili | 5,000/= kwa mwezi |
| 41 | Dahalia | 20,000/= kwa mwezi |
| 42 | Kituo cha Michezo | 5,000/= kwa mwezi |
| 43 | Uwanja wea Michezo | 10,000/= kwa mwezi |
| 44 | Washona Viatu:<br>Katikati ya Mji<br>Pembezoni mwa Mji | <br>3,000/=<br>1,000/= |
| 45 | Stoo za Mkaa | 10,000/= kwa mwezi |
| 46 | Mama lishe/ Baba lishe | 5,000/= kwa mwezi |
| 47 | Vituo vya kuoshea magari | 5,000/= kwa mwezi |
| 48 | Aina nyingine ya Biashara/ huduma | Ada itapangwa na kamati ya huduma husika na chanzo hicho kila itakapohitajika |

SEHEMU B

GHARAMA ZA UTUPAJI TAKA KWENYE JAA LA TAKA

| Namba. | Kiasi cha taka | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Chini ya tani moja kwa safari | 10,000/= |
| 2 | Tani moja kwa safari | 15,000/= |

____________

JEDWALI LA PILI

____________

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 19)*

GHARAMA ZA UBOMOAJI NA UONDOAJI WA MABAKI YA UJENZI

| Namba. | Eneo kwa mita ya ujazo | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Mita moja ya Mraba | 5,000/= |

____________

JEDWALI LA TATU

*(Limetungwa chini ya aya ya 31)*

KUFIFILISHA KOSA

Mimi…………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………… ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe kwamba mnamo tarehe…………… ya mwezi…………….. Mwaka ………………………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ndogo ya………… ya Sheria Ndogo ya (Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Songwe ya Mwaka 2024.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe. niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo Tarehe…ya Mwezi……………Mwaka…….
Jina………………………………...…..
Saini……………………………...….
Mbele ya:
Jina………………………………………….
wadhifa……………………………………
Saini……..…………………………………..
Tarehe: ……………………………………..

Nembo na muhuri wa Halmashauri ya wilaya ya SONGWE imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia Azimio Na SDC/ MB/09/2023 lililopitishwa na Mkutano wa Baraza la Madiwani kilichoketi Tarehe 02/1/2023 na ubandikwaji huo kushuhudiwa na;-

CPA CECILIA D KAVISHE
*Mkurugenzi Mtandaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Songwe*

ABRAHAM KAGULUKA SAMBILA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Songwe*

NAKUBALI

/

L.S

Dodoma,
30 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*